# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA NISHATI

## WAKALA WA NISHATI VIJIJI (REA)

# FOMU YA MAOMBI YA MKOPO NAFUU WA UWEZESHAJI WA UJENZI NA UENDESHAJI WA VITUO VIDOGO VYA BIDHAA ZA MAFUTA (PETROLI NA DIZELI) VIJIJINI

**MACHI, 2024**

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ulianzishwa kwa Sheria ya Nishati Vijijini, Na 8 ya Mwaka 2005 na kuanza rasmi mwezi Oktoba 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa iliyokuwa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003, Sheria ya Nishati Vijijini pia ilianzisha Bodi ya Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini.

Wakala wa Nishati Vijijii ni Taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Nishati, yenye jukumu la kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya nishati bora kwa lengo la kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi vijijini. Wakala wa Nishati Vijijini kupitia Wizara ya Nishati hufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wabia wa Maendeleo, Idara na Mashirika mbalimbali ya Serikali.

Katika kuhakikisha nishati bora na salama maeneo ya vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini, umeendelea kutekeleza majukumu yake ukijikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na mafanikio makubwa yameonekana. Wakala wa Nishati Vijijini pia unatekeleza miradi mbalimbali ya Nishati ya kupikia. Katika kuongeza upatikanaji wa nishati vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini pia una wajibu wa kuhakikisha nishati ya mafuta na petroli inayopatikana vijijini ni safi na salama.

Serikali ya Tanzania imeanzisha mpango wa kuwezesha ujenzi wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu vya bidhaa za mafuta (petroli na dizeli) maeneo ya vijijini ili kuondosha njia zisizo salama za uhifadhi wa mafuta hayo kwenye mapipa ndani ya nyumba na madumu ya plastiki, kuuza kwa kutumia chupa za plastiki ambapo ni hatari kwa usalama kutokana na uwezekano wa kutokea kwa milipuko ya moto na uharibifu wa mazingira.

Kwa kutambua hali hiyo na kwa kuzingatia moja ya malengo ya sera ya nishati ya mwaka 2015 ni kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati na kwa bei nafuu katika maeneo yote ya nchi kwa njia iliyo salama. Wakala wa Nishati umetenga fedha za kutoa mikopo nafuu kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo vidogo vya kuuzia bidhaa za mafuta (Petroli na Dizeli) vijijini. Mkopo huu utasaidia uwezeshaji wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu maeneo ya vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya mafuta kwa gharama nafuu na kwa njia salama na isiyo na madhara kwa mazingira.

Wakala unakaribisha waombaji wenye vigezo kuomba mkopo huu ili kuwezesha ujenzi na uendeshaji wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu maeneo ya vijijini.

**KIPENGELE NA. 1: TAARIFA NA VIGEZO VYA MWOMBAJI (MWENDELEZAJI)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1.1 | Jina la Mwombaji | | |
| 1.2 | Aina ya Mwombaji (Mtu Binafsi, kampuni au Kikundi) | | |
| 1.3 | Anuani ya Mwombaji | | |
| 1.4 | Barua pepe ya Mwombaji | | |
| 1.5 | Namba ya Simu ya Mwombaji | | |
| 1.6 | Namba ya Mlipa Kodi (TIN) ya Mwombaji | | |
| 1.7 | Jina la Mwakilishi/Mdhamini wa Mwombaji | Jina: | Cheo: |
| 1.8 | Anuani ya Mwakilishi/Mdhamini wa Mwombaji | | |
| 1.9 | Barua pepe ya Mwakilishi/Mdhamini | | |
| 2.0 | Namba ya Simu ya Mwakilishi/Mdhamini | | |

**KIPENGELE Na. 2: MAELEZO YA ENEO/MAHALI LA MRADI**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.1 | Jina la Kituo | | | | | |
| 2.2 | Eneo Mradi ulipo | Mkoa: | Wilaya: | Kata: | Kijiji: | Kitongoji: |
| 2.3 | Je, Kijiji kina kituo cha mafuta? | | | | | |
| 2.4 | Umbali wa kijiji kutoka kituo cha mafuta kilichopo karibu | | | | | |
| 2.5 | Umbali wa kijiji kutoka katika barabara ya Tanroad | | | | | |
| 2.6 | Namna ya kufika katika eneo la Biashara | | | | | |
| 2.7 | Ukubwa wa Eneo la Biashara (Mita za Mraba) | | | | | |
| 2.8 | Umbali wa eneo la biashara kutoka maeneo ya huduma za jamii | | | | | |
| 2.9 | Uko tayari kulipa bima ya majanga ya moto endapo maombi yako yatakubalika? | | | | | |

**KIPENGELE Na. 3: MAELEZO YA UJENZI**

Ambatisha Mchoro (Site Layout) ulio na vipimo unaoonyesha mpangilio wa vifaa na majengo vitakavyokuwa katika eneo la biashara ukizingatia matakwa ya Mwongozo wa mradi.

**KIPENGELE Na. 4: MAELEZO YA VIGEZO VYA BIASHARA.**

Ili Kukidhi kigezo hiki, ambatisha taarifa zifuatazo;

a) Barua ya mwombaji inayoainisha kiasi cha mkopo, lengo la mkopo, chanzo cha fedha za marejesho na mpango wa marejesho na dhamana ya mkopo;

b) Kwa mfanya biashara wa mafuta, kumbukumbu za mauzo ya mafuta kwa muda wa miaka 2 iliyopita (2022 na 2023);

c) Asiye na uzoefu wa biashara ya mafuta, kumbukumbu ya uzoefu kwenye biashara nyingine yeyote anayoifanya;

d) Kama kikundi ambacho kinaomba mkopo, barua kutoka mamlaka zinazoonyesha madeni na uwezo wao wa kukopa kutoka serikali ya kijiji na mamlaka zinazowasajili;

e) Barua inayothibitisha mauziano na msambazaji wa mafuta mwenye leseni ya EWURA aliyekaribu kwa ajili ya kununua mafuta.

**KIPENGELE Na. 5: VIGEZO VYA MKOPO**

| | | |
|---|---|---|
| 5.1 | Jina la Eneo la Mradi | |
| 5.2 | Tarehe ya kuanza ujenzi | |
| 5.3 | Tarehe ya kukamilisha ujenzi | |
| 5.4 | Aina ya Huduma (Petroli au Diseli au vyote) | |
| 5.5 | Gharama ya mradi | |
| 5.6 | Kiasi cha Mkopo | |
| 5.7 | Tarehe kukopa | |
| 5.8 | Muda wa Mkopo | |
| 5.9 | Tarehe ya kuanza Biashara | |
| 5.10 | Kiasi cha mauzo (lita) kwa Mwezi | |
| 5.11 | Gharama za Uendeshaji | |
| 5.12 | Tarehe ya marejesho ya kwanza ya mkopo | |
| | Dhamana ya mradi | |

| | | |
|---|---|---|
| 5.13 | Eleza umuhimu wa kuwepo kwa uhitaji wa huduma ya kituo cha mafuta ndani ya eneo hilo | |
| 5.14 | Ainisha taarifa za kibiashara (idadi ya vyombo vinavyotumia mafuta katika eneo husika, bei za sasa za mafuta (petrol na dizeli) katika eneo husika) | |

**KIPENGELE Na. 6: VIGEZO VYA KITUO CHA KUUZIA BIDHAA ZA MAFUTA**

| NA | KIPENGELE | MAELEZO MAFUPI YA KAZI | IDADI | GHARAMA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jengo la Ofisi | Mita za mraba 16 (4mx4m); Bati geji 28; tofali za kuchoma au sementi; vyoo viwili (2), sakafu ya sementi, Milango, Madirisha na rangi. | 1 | |
| 2. | Paa la kituo cha mafuta (canopy) | • Mita za mraba 21 (7mx 3m), Bati la geji 28; paa la chuma lililosimikwa kwenye kitako cha zege;<br>• Kitako kijengwe kwa sementi na kiwe na eneo la mita 4.5 sqm ( 3 x 1.5) na kimo cha mita 0.15 | 1 | |
| 3. | Matenki ya kuhifadhi mafuta | Tenki moja (1) la kuhifadhia mafuta. Kama utauza aina zaidi ya moja ya mafuta, matenki yaongezeke sawia. Tenki liwe na ujazo wa angalau lita 4,500 au 5,000; Tenki lijengwe kwa kutumia Chuma cha carbon (carbon steel) ; Tenki lipakwe kemikali ya kuzuia kutu, Tenki lijengwe chini ya ardhi na kusakafiwa juu kwa zege lenye unene wa inchi sita (6). Eneo la kushushia mafuta liwe na ukubwa wa mita za mraba 16; | 1 au 2 | |
| 4 | Mfumo wa kutenganisha | Mfumo wa kutenganisha maji na mafuta uwe na chemba tatu | 1 | |

| NA | KIPENGELE | MAELEZO MAFUPI YA KAZI | IDADI | GHARAMA |
|---|---|---|---|---|
| | mafuta na maji (Oil/Water Separater) | kama ilivyoanishwa kwenye **kiambatisho Na. 4 katika Mwongozo** | | |
| 5 | Pampu ya mafuta | Pampu ya mafuta ya kawaida yenye mikono miwili (2); | 1 | |
| 6 | Vifaa vya zimamoto na maji safi | Kituo kiwe na Miundombinu ya maji safi na zimamoto kama iliyoanishwa katika mchoro **kiambatisho Na. 2 katika Mwongozo** | Seti moja | |
| 7 | Vifaa vya umeme kwenye kituo | Jengo pamoja na kituo kitandazwe mifumo ya umeme kulingana na viwango vya TANESCO | Seti moja | |
| 8 | Vifaa vya usafi wa kituo | Kituo kiwekwe Miundombinu ya usafi wa mazingira *(WC and Septic Tank System)* | Seti moja | |
| 9 | Vifaa vya uondoaji maji ya mvua | Kituo kiwekewe Miundombinu ya uondoaji maji ya mvua *(Storm Water Drainage System)* | Seti moja | |
| | | | **JUMLA** | |

**KIPENGELE Na. 7: VIAMBATISHO**

Nyaraka zote zilizoelezwa katika Mwongozo ndani ya vigezo vya Mwombaji (Mwendelezaji), vigezo stahili vya Eneo/Mahali, vigezo vya ujenzi, vigezo vya kifedha na uzoefu wa biashara kwa Mwombaji, zinapaswa kuwasilishwa pamoja na fomu hii ya maombi iliyojazwa kwa ukamilifu unaohitajika.

**KIPENGELE 8: MAELEKEZO, MAWASILIANO & UWASILISHAJI WA MAOMBI**

Maelekezo na taarifa zaidi zinapatikana katika Mwongozo kupitia tovuti ya Wakala wa Nishati Vijijini ambayo ni www.rea.go.tz

Maombi yaliyokamilika pamoja na viambatisho vyake vitawasilishwa kupitia njia zifuatazo:

a) **Njia ya Posta au kuleta ofisini;** tumia anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu,
Wakala wa Nishati Vijijini
Jengo la Wakala wa Nishati Vijijini (REA),
Barabara ya Medeli,
S. L. P. 2153,
**DODOMA, TANZANIA.**

**MUHIMU:**

Juu ya bahasha baada ya anuani ya Wakala iandikwe ***'Maombi ya Mkopo kwa Ajili ya Ujenzi wa Vituo vya Mafuta Vijijini'***

b) **Njia ya Mtandao,** tumia barua pepe; vituovyamafuta@rea.go.tz

**Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na wafuatao:**

Jina: **Mha. Kelvin Tarimo**
Namba ya Simu: 0713 230358

Jina: **Mha. Ramadhani Mganga**
Namba ya Simu: 0754 909237